MAHUBIRI N°3: UFUNUO 14:6-10

(*Ilihubiriwa jumapili tarehe 10 novemba 2002, huko Locodjro, Abidjan-Cote d'Ivoire / www.matth25v6.org*)

[Ndl: Ndugu Filipo anasoma Ufunuo 14:6-10]…unaona? Injili ya ufalme wa mbinguni kila mara hutoka mbinguni kupitia malaika, lakini kuna injili ingine itokayo jehanam kupitia seminari na shule ya uchungaji. Kwa sababu Mungu hujaza moyo lakini ibilisi hujaza kichwa. Kumbukeni ginsi gani tarehe 24 aprili 1993, mlio wa sauti yake uliingia moyoni mwangu na nikaanguka kama mufu. Unaona? Ni ibilisi aliye anzisha shule ya uchungaji. Kwa maana nikimtuma mtu kumwita mke wangu aliye kijijini, yeye hana lakupokea kutoka mwingine. Ni mimi peke ninaye lakumwambia kuhusu yale anapashwa kumwelezea mke wangu na ninajua kwamba mke wangu atamwamini. Unaona? Shetani na wana wake wakamate hizo shule, masomo ya teolojia na internet, [lakini] mimi na nyumba yangu tutabaki na ufunuo wa unabii. [Kusanyiko linasema « *amina*! »]. Na baada ya shule ya uchungaji, seminari na vieti vya teolojia, wakati hawa wadanganyifu, hao wana wa ibilisi wanasimama kwa sakafu, wanasema: « *Ee Mungu! Nisionekane lakini useme kupitia mimi* ». Unaona? Ni kuchanganyikiwa! Ungejua kwamba Mungu anaweza ku kuondoa na kusema kupitia wewe, sasa ni kitu gani ulikwenda kutafuta katika shule la uchungaji?

Shule la uchungaji ni tu pahali ambapo watu huenda kujifunza ufundi wa kucheza na saikolojia ya watu. Unaona? Wanajifunza mwenendo ya kila mtu na namna yake. Ni hayo yote inaitwa uchawi. Ni ile wanayo ificha ili watu wasielewi.

Vema, Biblia inaeleza kwamba hakuna jambo ambalo halitawekwa wazi kwa mwanga wa mchana. Mungu aliifanya kwani wakati wa urudisho ulitimia lakini kwa bahati mbaya wale ambao ilitayarishwa kwao walikuwa tayari wamelewa kwa namna hawangeweza kutofautisha mema na mabaya, Roho ya Mungu na ile ya ibilisi, neno la Mungu na teolojia… Ni basi kwa udanganyifu hii umbo la shetani laitwa kanisa, na kugeuka kwa ghafla laana kwa nchi na jambo la kasirani yote ya Mungu. Hata ikiwa wakati Mungu anamwanga kikombe cha mateso juu ya nchi moja, makanisa wanajiharakisha kutafsiri mambo yale ili wasimamishe imara mwovu katika njia yake. Ninajiuliza ni kwa azabu gani itastahili makanisa wahukumiwe siku ya hukumu! Mufahamu kwamba Mungu angelikuwa mwongozi wa makanisa hizo, hawangeli weza kuomba wakati moja na wa buda, wamahikari, waislamu, wafumu, wachawi, wakati wa sadaka ya maji na ya michezo za vita… na ikiwa waliifanya, iliwabidi wajieleze kupitia hiyo televisheni mbovu na yenye kuoza, hizo barabara za maakida na uakida, magazeti zinazoonyesha wanawake uchi, usawa na michezo chafu, kugawanyia watu ma kapoti, usawanisho wa jamaa. Unaona? Pahali zambi inashimikwa kisheria, inabidi Kanisa isema. Ikiwa kapoti zinagawanywa kwa wanafunzi, maaskari na wengine na makanisa wanabaki kimya, basi inawabidi pia kuache kusali na kama sivyo wao ndiyo maadui kabisa wa nchi yao. Zambi ya mtu anayetumia kapoti (ao mpila) ao dawa za kupanga uzazi ni sawa na ya yule anaye ondoa mimba. Ni hasa juu ya makanisa [ndio] azabu zinatumwa sawa zamani ilivyokuwa juu ya miungu za Misri. Unaona? Siwakatishe tamaa lakini ni kwa bure munaomba. Mungu alijisimamishia watumishi kwa kufanya hukumu kama vile zamani alisimamisha mtumishi wake Nebukadneza juu ya Israeli. Siyo Mungu ndiye anaye amuru yote inayotokea duniani?

Kama Yosefu, watu weusi waliyochukuliwa toka Afrika, pia wana kondoo walipokuwa wakikimbia mbwa mwitu za mateso ya kirumi wakakutana juu ya nchi mpya, yaani Amerika. Mungu akawabariki, akafanya ndugu zao wote, Dunia nzima, waanguke kifudifudi mbele ya shauri lao kupitia UMOJA WA MATAIFA kwa sababu nyuma ya papa, ilikuwa Yosefu. Kama inavyoonekana katika kitabu cha Mwanzo na katika Ufu.13. Unaona? Wao basi waliyokuwa wana kondoo, wajukuu wa wajukuu wa wakristo, wanaofanya kiapo juu ya Biblia, wakageuka kuwa joka moja inayovunja vipande vipande, inayo ripua, wanao komesha kupitia kufungia nchi jambo fulani. Kuliko kutumia jamaa yake ngano kwa bure ili wapate kuishi, wanatuma kwao silaha ili wauane wenyewe. Wanawatumia wa Osborn, Morris Cerullo… kwa kudanganya watu wa dunia. Na wanafurahia kusema: "*Mungu abariki Amerika*". Ikiwa Mungu anaweza kubariki Amerika ninayo tazama halafu inamubidi kujuta kwa nini aliharibu Sodomo na Gomora. Munaona? Mungu akibariki hii "Cote d'Ivoire[1]" ninayoona halafu inamupasa kujuta kwa nini aliharibu Sodomo na Gomora. Na siku ya ufufuko, Mungu analazimishwa kuomba msamaha kwa watu wa Sodomo na Gomora. Unaona? Na tarehe 11 mwezi wa tisa, nilisema nikipungukiwa tumaini: "*imefanyika*" na nilisema kwamba ni ile ilisemwa na mjumbe wa wakati wa mangaribi kabla nitazame hizo picha. Rehema kwa taifa hilo, watafanya nini? Na tangu sasa woga na wasiwasi zitakaa pamoja na watu hawa. Kwa maana kuliko kutumika kwa wema, walitumika kwa kuangamia kwa mwovu. Jibu si kutafuta kukamata Alkaida, ao wanao tia woga duniani ambao hizo ni fimbo nzuri za Mungu lakini inafaa kugeuza maisha kwani Mungu anaweza kusimamisha fimbo kutoka pahali pote, mvua kubwa ya upepo, tetemeko la dunia, nchi kujaa maji, hata hamujui kwamba magonjwa ngumu zaidi kuliko ukimwi zitakuja. Hamujui kwamba isiyo na mamlaka ya kuua itaanza kuua? Na Mungu atasimamisha yote kwa mtu yeyote au taifa lolote linalo pendezwa na zambi pia na manabii wa uwongo. Ni kwa ajili ya hiyo Mungu aliharibu dunia kwa siku za Noa. Makanisa zilikuwa na wa Osborn, wenye kudanganya, watu wenye sifa wanaokubaliwa na watu. Na njia zote za wokovu ziliharibiwa. Tazameni Mwanzo 6:11-12: « …*dunia ikaharibika mbele ya Mungu, na dunia ilijaa na jeuri. Mungu akaona dunia, na tazama, imeharibika; kwa sababu wenye mwili wote wamejiharibia njia duniani* ». Angalieni vizuri [jambo] hili: « …*ikaharibika mbele ya Mungu* ». Hapana mbele ya watu lakini mbele ya Mungu! Kwa macho yao, wao ni katika kweli, hawaoni ubaya kwa yale wanatenda! Na ni pale Mungu akawasimamishia mtu mmoja mdogo, asiye na elimu ya teolojia, ambaye mahubiri yake iliwasumbua. Lakini Noa akahubiri katika jangwa ya kweli.

Watu wanatambua kwamba tuko kwa wakati wa Noa. Wahubiri wote wanatambua kwamba tuko kwa wakati wa Noa. Makanisa wanatambua kwamba tuko kwa wakati wa Noa… Lakini Noa yuko wapi? Ni swali ndogo ambalo hawajiulizi. Sasa, namna gani twaweza kuwa kwa wakati wa Noa bila Noa? Oh! Ninyi wana wa Mungu, musitafute wachungaji wakuu, mitume na manabii lakini tafuteni Noa! Oh wachungaji wadogo wadogo! Oh wa majusi wadogo wadogo! Musikwende ngambo ya Yerusalema lakini nendeni Bethelehemu! Musikwende kwenye makanisa za Herode, musikwende kwa wale wanao jiita watu wakuu wa Mungu, nendeni kwa musermala Yosefu.

Na ikiwa Noa amekubaliwa, mimi pia nitakubaliwa, ni juu ya ile ninasimama. Na ninashangaa kuona watu wanaokiri jina la Yesu Kristu wanatamani wafike siku moja Amerika. Vijiji vyenu si bora kuliko Los Angeles na Hollywood? Jehuri inatokea wapi? Hizo nyoka na nge juu ya mikono, hizo nywele za uwongo? Kwa namna munatamania kwenda Ulaya na mangaribi, vivyo hivyo nafsi yenu inaona kiu ya zambi na jehanamu! Kwani wote waliyo huko ulaya hata Amerika ambao wamejazwa Roho Mtakatifu wanatamani kuwa kwa pahali yenu hapa Afrika, mbali na yale macho yao yanaona kule.

Mnyama wa kwanza ya Ufu.13, Vatikani, alichafua dunia kupitia kanisa katolika. [Na ninawaambia mutege sikio juu ya Vatikani. Ujumbe moja utatikisa dunia. Hiyo wakati imetimia sasa na silaha, ni roho iliyo katika Al- kaida. Na dunia itasema: nani alifanya

hivi? Unaona?]. Mnyama wa pili, Amerika, yeye mwenyewe picha ya Vatikani, aliharibu dunia kwa makanisa za kiprotestanti na za kiinjili ambazo pia ni sura ya ukatolika, wote wakitumika chini ya alama ya mnyama, roho iliyokuwa zamani katika Babeli na iliyopita kwa Babiloni, kisha kwa wa Medi na wa Persi, kisha kwa utawala wa wayunani, na kwa mwisho kwa utawala wa warumi na kwa kanisa katolika inayotoka Roma. Na hapo, hiyo roho ikapitishwa kwa MAREKANI na kwa makanisa za kiprotestanti na za kiinjili na kwa mwisho kwa wabranhamisti.

Na kusema Cote-d'Ivoire[1] ndiyo Yerusalema mpya, ni kumtukana Mungu na kiti chake cha enzi! Na ikiwa Cote-d'Ivoire ni tembo ya uchumi na politika, yeye pia ni popo kiroho na ile ilionyeshwa wazi tangu wakati moja kwa macho ya dunia. Ndege inayo ruka, inakula na kufanya choo kupitia kinywa, inalala ikisongwa kichwa ikiangalia chini. Ndege inayo ruka usiku, ina manyoya na meno: Kiumbe cha mambo mbaya na ni hivyo kwa hao wanaojidai kuwa wakristo. Wakatolika, waislamu, wabuda, waprotestanti, wakiinjili, wachawi… walikusanyika pamoja kwa kuomba mungu wao. Ujinga wa wakristo umeonekana. Moyo na umbo lake zimefunuliwa. Je! Nitakubali nitolee ili nchi inayojidai kuwa haina dini iishi? Mungu ni katika kujitafutia utukufu? Mungu anayesema kwa mifano si yeye mwenyewe aliye weka popo katikati ya mji, katikati ya Abidjan, katikati ya Cote d'Ivoire[1]? Kwa nini? Ni mfano wa kiroho ya kidini ya nchi hiyo. Ni *ndivyo asema Bwana.* Siku moja nilikuwa nikihubiri juu ya mlima, na nikasema kwamba Cote d'Ivoire ilistahili zaidi kuliko ukimwi na mtu mmoja akapiga kelele: « *ikiwa ukimwi ni ndogo, Mungu atume joka, tuko tayari!».* Siku zilizo fwata, nchi ikapigwa, damu ikamwangika. Kwa hakika joka zilishuka. Ikiwa zambi zinawataka na sasa munafanya kiburi munapo kemewa, Mungu atawapandishia wa Ben- Laden waliyo wekwa na mamlaka ya unabii na ya uungu. Mungu ambaye mbele yake ninasimama ni yeye anaye timiza mipango yake juu ya watu wa dunia. Mulionyesha kwa uso wa dunia namna gani mwaweza kufanya ubaya zaidi kuliko Zaire ao Shala Mwana… Niombe Mungu basi ili barabara za maakida ziishi? Ili makanisa na manabii wao waishi? Ikiwa nitafanya hivi, nafsi yangu isiishi tena na milango za Hadeze zinishinde. Lakini ninaomba kwa ajili ya wachaguliwa ili maji isiwatelemushe na wakusanyike kwa ajili ya uzima wa milele na imani yao isipungukiwe.

Lakini dunia itaenda kwa mateso juu ya mateso. Na itafikia kiwango moja, kwa kusalimu, mutu hataweza kushika mkono wa ndugu yake au wa rafiki mpendwa wake ili asiambukizwe na ugonjwa. Watu watatembea pasipo kugusana. Mutasikia ikisemwa: « ninaogopa kusafiri katika gari ili nisiambukizwe». Unaona? Mwenye haki atamwambia mwovu: « kwenda uonyeshe uchi wako kwa mchanga wa pembeni ya bahari! ». Na mwovu atajibu: « sitakwenda! ».

Vema, Biblia inasema nini? Mat.24:24 inasema nini? Biblia inasema ya kwamba, kama wakati haungefupishwa, hakuna mtu angeliweza kuokolewa. Lakini tunapoona kazi na kuzidishwa kwa makanisa, tunaweza kufikiria kwamba Bwana akichelewa kuja, watu wote wataokolewa. Musidanganyike mpaka kwa hali hiyo! …na musinitazame kama hatari kwa makanisa zenu sababu ya faida zenu lakini munitazame kama neema. Wananikamata kama nabii wa uwongo, mpinga Kristo, mtume wa shetani, mahubiri nivaquine …bila kuonyesha uwongo gani nilisema. Nyinyi munaohubiri teolojia na mambo mengine, nendeni basi paradiso! Baada ya hayo Noa, Musa, manabii, mitume na mimi, sisi tuliohubiri Injili inayotoka mbinguni, tutaenda jehanamu. Wana wa upotevu wanaopeleka nafsi nyingi kwa upotevu!... Munitukane nabii wa uwongo na mpinga Kristo lakini Mungu anawangojea hukumuni!

Lakini Bwana aliahidia katika Mat.13:24-30 kwamba wana wa Ibilisi na makanisa zao watafungwa kwa vikundi vyengi kwa kuchomwa lakini wachaguliwa watakusanywa katika gala moja. Kulikuwa imani nyingi na miungu nyingi huko Misri na Mungu aliwatoa wana wake akitumia hukumu. Katika wingi wa makanisa za Israeli, palikuwa na wafarisayo, wasadukayo, wayunani, waherode, wazelote,… Wote walikuwa katika uwongo na bwana akawatoa wachaguliwa akifanya hukumu juu yao. Na mbele ya kuchukuliwa, kufuatana na Mat.24:31 na 1Tes.4:16 wachaguliwa watakusanywa kwa sauti ya baragumu, pamoja na Ufu.14:6-10. Na kila mara ni ile Yesu Kristo iko akifanya. Na mahubiri hii ni kwa kuanguka kwa wamoja, na kusimama kwa wengi. Ni ile ile garika iliyo mwokoa Noa, ndiyo iliyoangamiza dunia. Ni ujumbe huu utakao wahukumu.

Ijapokuwa mafundisho [yao] ni tofauti, makanisa yanajiunga katika miungano na nilisema kwamba ile ilikuwa ni wanyama, wajoka wa vichwa vyengi, kila kichwa ikiwa mfano wa kanisa moja na ikiwa na pepo chafu, na lugha yao ikiwa teolojia ya ile kanisa. Yeyote anayepatikana katika moja ya makanisa hizo amekwisha kupokea alama ya mnyama, ni kusema roho, pepo chafu ya mnyama. Mumezaliwa kwa ile roho na ni kwa ile roho munasema kwa lugha, munatoa unabii,… ikionekana kuwa Roho Mtakatifu.[Ni yeye] Anachunguza mwili wako, nafsi na roho yako. Na unakuwa kabisa katika hali ya wafarisayo mbele ya Bwana au katika hali ya mkatoliki aliye na mishumaa, sapuli, sanamu, uvumba, msalaba na maji ya baraka mikononi na akijiwazia katika kweli. Ile ile alama, ile ile pepo mchafu ya kuleta moyo mgumu inayoshika mnyama [kanisa katolika] ni ile ile alama inayoshika picha yake, binti zake.

Mtu akisema: "*mimi ni mubatisti, ndugu wa ujumbe, mulutheri,…*", inafaa kufahamu pale: "*mimi ni mpinga Kristu, mimi ni mtoto haramu, mimi ni…*". Alama kwa mkono ni kutenda, kufanya matendo katika njia ile. Na dunia yote imekwisha kuipokea. Hakuna mfalme au rais duniani ambaye hakwenda wala hana nia ya kwenda Vatikani, hata Arafat, waarabu na waislamu. Kwani, katika Mat.4:8-9, Yesu- Kristo alipokataa cheo cha utawala wa hali ya juu sana duniani, mtu mmoja aliipokea. Na Biblia inasema kwamba huu mji mdogo wa Vatikani una utawala juu ya watu wanaokaa duniani na kwamba siku moja mkono moja usiyoonekana utaipiga. Ufu.17:18…

Kila kanisa inajidai kuwa na Roho Mtakatifu na kila moja wao ana maoni yake juu ya ubatizo, uungu wa Yesu, kutangulizwa, zambi ya asili, huduma ya mwanamke, kitambaa, na vivi hivi. Mchungaji wa kanisa la wametodisti hawezi kuwa mchungaji kwa kusanyiko la miungu, ao kwa wabatisti,… Hii ni Roho Mtakatifu gani inayo jipinga yenyewe? Na hata hivi hamutafuti kweli lakini munazungumzia utakaso na paradiso. Munafanya nini basi na Biblia ilyo mikononi mwenu? Hivi, ni kwa wokovu kabisa munakwenda kanisani? Lakini Mungu akiokoa mubatisti moja, mupentekoste, wa uamsho au wa mkutano ya miungu, namna gani anaweza ku wahukumu wafarisayo, Yuda, Kaina? Namna gani Mungu anaweza kuhukumu mafundisho ya wafarisayo na ya wasadukayo na kukubali ile ya kwenu? Kufwatana na Mat.16:5-12 Yesu anasema hiyo ni chachu.

Mungu akimupa Roho Mtakatifu mubatisti, mupentekoste, wa mkutano ya miungu,… itakuwa vipi kwa wabuda, na waislamu? Unaona? Ninawasihi kwa jina la Bwana Yesu Kristo, acheni kuchoma uvumba juu ya mapepo wachafu! Acheni mazabahu na ndama ya zahabu. Huduma siyo kazi ambayo ni lazima kujifunza au kukamilisha katika seminari ya mafunzo. Acheni kutengeneza wachungaji katika kampeni zenu za uchungaji. Mungu anatoa huduma toka mbinguni na anafatilia mwenyewe namna itatendeka bila usaidizi wa mkono wa mwanadamu lakini kwa Roho Mtakatifu. Ninyi ndugu zangu wachungaji, manabii, wa reverenti, waprezidenti…ninawaalika katika jina la Yesu Kristo! Tubuni! Hepukeni hadeze kwani, ni heri kupata haya mbele ya watu kuliko hadeze. Siwahubiri mafikiri lakini ninasema nanyi kwa jina la Bwana Yesu Kristo. Kama Yeremia 28 na 1Fal.22, nilipewa kuona hukumu ya Mungu na ku itamka. Haizuru kanisa gani wala mtu gani, hata iwe nani asiwadanganye!

Cheo kanisani isikushike. Tambueni siku yako ya kutembelewa kwani ukakosa baragumu ya kusanyiko, basi unangoja nini? Pigeni basi magoti mpaka Mungu aseme nanyi kama sivyo hukumuni hamutasema kwamba hamukuambiwa! Sivyo?

Ikiwa Israeli aliye wa Mungu toka kuzaliwa hafahamu misemwa ya unabii, namna gani ninyi muliyo wa Mungu kwa kuwekwa mamlaka mutaweza kufahamu? Lakini jambo moja ni la kweli: watu wawili wanao jidai kuwa watu wa Mungu hawawezi kushika misemwa tofauti na kutenda tofauti. Wakati wayahudi walitoka kwa kuchukuliwa huko Babiloni, mubenyamina kama Paulo aliweza kupatikana katika ukuhani. Kukasikika majina mpya: rabini, mfarisayo,… kama ilivyoandikwa katika 1Fal.12:31 na 2Mambo ya siku13:9, mtu akiwa na mapato ya pesa, analipa mafunzo na anakuwa kuhani kama tunaiona leo. 2Mambo ya siku13 inasema: *"hamukufukuza makuhani wa Bwana, wana wa Haruni, na walawi? Na mukajifanyia makuhani kama wanavyofanya watu wa nchi nyingine; Ye yote aliye kuja na ndama na kondoo dume saba, ili awekwe kuhani, alikuwa kuhani ya Yule asiye kuwa Mungu…"*. Unaona? Siyo tena uchaguzi wa uungu lakini jambo la akili na pesa. Makanisa zilipo toka huko Babiloni ya kiroho, ukatolika, ambapo zilichukuliwa, kulianza kusikika majina kama: reverenti, presidenti, bishop,… majina ya makufuru. Walirudia na mafundisho ya sharti, kanuni za imani, mafundisho pamoja na miungu ya wababiloni. Watoto wa Nimurodi, mwana wa Beliali walijifanyia utawala waliyoiita *"kanisa"*. Ilikuwa ni wafalme pasipo taji, ni utawala pasipo serkali, wanyama wa mapembe mbili au tatu kufuatana na ile ya wababiloni. Na wakiongozwa na mpango moja, wiko wakijenga minara za babeli ijapokuwa kuna mchanganyiko kati ya misemwa yao, mafundisho: [lakini wanafanya] miungano ya makanisa. Kupima Mungu. Kila mmoja alikuwa na mapembe tatu: mamlaka ya politika, pesa na dini.

Ukiwa nabii na sasa huoni maneno haya: *"mtangulizi wa mpinga Kristo"* juu ya uso wa hao ma prezidenti wa makanisa, sasa ujiulize wewe ni nabii wa nani. Sijitazami kama nabii lakini najua jambo moja: niliona imeandikwa mbinguni hukumu ya Mungu juu yenu na hakuna anayeweza kuipinga. Na wana wa Ibilisi wanasimama mbali kwa kusema: *"yale unayo yasema ni kweli, sisi pia Mungu alitufunulia"*. Ikiwa kweli Mungu aliwafunulia, siyo kwa ajili ya kanisa lingine lakini mutakuja kwa neno lake na kwa Kanisa lake …

[Katika kijiji changu, amekufa kama aliyepigwa na malaika mtu mwenye sifa na kujulikana wa kusanyiko la miungu: *Muzee Nando*. Kupooza ambayo haikutii maombi na kulia mbalimbali ya walio wa kwake. Ile ndiyo mushahara wa miaka nyingi ya uchawi katika sanduku inayoitwa kwa jina la: *kusanyiko la miungu* na ambayo Katadji ni kitanda cha kuwalea. Na nilisikia kwamba alitengeneza maisha yake mbele ya kufariki. Basi hakufariki akiwa bado angali mwanamemba wa kusanyiko la miungu? Ikiwa alizuiza mwili wake, ni vizuri lakini ni vipi kwa nafsi yake na ile roho takatifu ndani mwake? Aliacha hiyo mahubiri ya sharti, kanuni za imani, sanamu na teolojia ya wa kusanyiko la miungu mbele ya kufariki kwake? Ikiwa yeye atakwenda mbinguni, dini ya ukristo ni ya uwongo! Unaona? Huyo Nando alidanganya kabisa, alipofusha, alichuna na kutuma nafsi nyingi katika hadeze, hata hadeze yake ilianza hapa chini]*.munaweza kuwa hamukubaliane nami au munanipiganisha kwa sababu ninawaambia kweli lakini siku moja, mutasema kama huyu askari mrumi: *"hakika mtu huyu alitumwa na Mungu aseme nasi"*

Na moja ya sababu zinazo leta watu kama hao wasikubali ujumbe wa wakati wao ili waokolewe, ni kwamba wengi wa wale waliyodanganywa nao tayari wamekufa na wanawangojea kule mbinguni; na ni lazima wakwende kujibu mbele ya Mungu kwa ajili ya nafsi zile. Basi Mungu hawezi kubali wao wabadilike hapa duniani. Mungu angekosa haki ikiwa Dion Robert atakwenda katika paradiso ijapokuwa wabatisti wengi tayari wamekufa. Unaona? Ni hivi!

Kwa kumaliza, napenda kusema hivi: kwa mwaka 1995, malaika wa shetani alinionyesha ufunio nyingi na siku moja nilimwambia dada moja: *"ulifanya uasherati jumatatu iliyopita na askari mmoja. Baba yako anamjua kufuatana na yale niliambiwa"*. Dada huyo Alikubali na nilifikiri kwamba ni Mungu [aliye nionyesha]. Siku ingine, nilimwambia ndugu mmoja kwa jina la DEZIRE: *"Tutakapo fika kwa ndugu Edware, atatupatia hembe mbili, yangu itakuwa ya kuoza na ataibadilisha na dole mbili ya ndizi"*. Mambo yalitendeka sawasawa. Na ninakumbuka kwamba kwa mambo haya ya kishetani, niliwakwaza wandugu wawili ambao niliwaomba msamaha. Kwa mwaka moja, niliona ufunuo nyingi za namna hii na hakuna hata moja kati yao iliyo kosa kutimia. Washuhuda wangali hai. Utukufu, heshima na huduma kubwa ya unabii iliwekwa mbele yangu kama kwa Kacou Severin na hao manabii lakini Bwana akanisaidia na akanielimisha kwa ajili ya uzuri zaidi wa huduma ambayo ilikuwa lazima niifanye mbele ya uso wake. Na nilitubu mbele ya watu wote na nikakubali kwamba hizo ufunuo ijapo zilikuwa haki, zilitoka kwa ibilisi. Nilipata haya lakini nilipendelea haya mbele ya watu kuliko hukumu mbele ya Mungu. Lakini siku moja hiyo zawadi itatumika kutoka kwa Mungu mwenyewe.

Hakuna mtu hatammoja, haizuru nani, anayeweza kuwa na hekima kabisa kwa kuponyoka mwenyewe [hukumu], kama sivyo, mmoja wa manabii [wa leo] angeweza kuifanya. Siwezi tia wazi zowezi za 1993 kwa leo lakini ninasema kama aliye na mamlaka kwani nilisimama katika shauri la Mungu. Mukubali kukemewa! Kwani kile munachofurahia si lazima kile Mungu pia atakifurahia. Mtume Paulo alitaka kupanda karibu na mitume ili achunguze yale alikuwa akihubiri kufuatana na wagalatia2:1-2. Ulrich Zwingli aliifanya pamoja na Martin Lutheri na akasema: *"Niliamini sawa na Lutheri kabla nimuone"*. Kwa mwaka 1536, mpinduzi mkuu Giyome Farel akaomba Yoane Kalvini amsaidie kwa urudisho wa Kanisa la Geneve. Na ninyi? Muna roho takatifu gani? Munajitwalia makanisa! Mujitambue! Kwani njia Fulani ni nzuri kwa macho ya mwanadamu lakini mwisho wake ni upotevu.

[]* iliongezwa februari 2005

MAWASILIANO: Ndugu Filipo:+ 225-0252-0252 E-mail: kacou.philippe@yahoo.fr
Upate mahubiri katika site ya: www.matth25v6.org